



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO



Simu Na. +255(028) 2820137
Fax Na. +255(028) 2820137
E-mail.ded@kakonkodc.go.tz
Tovuti: www.kakonkodc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P 03,
KAKONKO.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na. HW/KNK/S. 40/VOL. II/29

06.03.2023.

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, kupitia kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/358/01"C"/146 cha tarehe 16 Januari, 2023 kilichotolewa na Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anapenda kuwatangazia wananchi wote wa Tanzania wenye sifa za kuajiriwa katika Utumishi wa Umma kuleta maombi ya kazi kwa nafasi ya Mtendaji wa Kijiji III kama ifuatavyo:-

Mtendaji wa Kijiji III – Nafasi 1

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Afisa masuuli na Mtendaji wa shughuli zote za Kijiji.
- ii. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, Mtunzaji wa Kumbukumbu zote za Kijiji za vikao vya Kijiji pamoja na hati ya kuandikishwa Kijiji, mali za Kijiji na rejesta ya Kijiji n.k'
- iii. Kuratibu na kusimamia na kuhamasisha upangaji na utekelezaji wa shughuli zote na Mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Kusimamia ulinzi na Utawala Bora wa wananchi (Mlinzi wa amani) katika Kijiji.
- v. Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo katika Kijiji.
- vi. Kupanga na kuhakikisha kupitishwa kwa ratiba za Vikao vya Mkutano Mkuu na Halmashauri ya Kijiji.
- vii. Kuandaa taarifa mbalimbali za Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya mkutano Mkuu wa Kijiji.
- viii. Msimamizi wa mapato na kodi za Kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya mshahara TGS B, Tsh 450,000 hadi Tsh 549,000. Atanza na Mshahara wa Tsh 450,000= kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI

Wahitimu wa kidato cha nne au sita waliohitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika (Tech. Level 5) au kinachofanana na hicho mojawapo ya fani zifuatazo; Utawala, Maendeleo ya Jamii, Sheria, Uongozi na Fedha kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali


Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P 03,
KAKONKO.

MASHARTI YA JUMLA

Mwombaji anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo kikamilifu.

- i. Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45, bila kujali jinsi ulemavu, kabila, dini au hali.
- ii. Aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Maelezo Binafsi (CV) yaliyojitosheleza kwa maana ya taarifa na mawasiliano. Pia aambatanishe picha 1 "Passportsize" iliyochukuliwa hivi karibuni na nakala za vyeti vya Taaluma (Academic) na Weledi (Professional). Transcript "Testimonials" na "Provisional Results" au Statement of Results havipokelewi.
- iii. Maombi yawasilishwe kabla au mnamo tarehe 17/04/2023 saa 9:30 Alasiri. Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda uliopangwa hayatafanyiwa kazi.



Ndaki S. Mhuli
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KAKONKO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALAMSHAURI YA WILAYA
KAKONKO

**NB: Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti ya HALAMSHAURI :
www.kakonkodc.go.tz**